

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
28 Juni 2008**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frank Peter Rwechungura
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Jumanne Idd Selemani
Paulo Atibu Hatibu
Sudi Saidi Ramadhan

Mradi wa usalama barabarani - Wamba Memorial Fund

Wakati wa mkutano wanachama walipitia manual kutafsiri. Elaine atachapa na tayarisha.

Kwa sababu training of trainers ni wiki tatu mbele tu, tulikubali kuanza kualika washiriki. Tutaalika mtu moja au watu wawili kutoka HUWATA, Chuo cha Usafirishaji, Traffic Police na walimu wa shule, na tutaandika barua ya kualika. Tulikubali kwamba wanachama 10 wa UWABA wanaweza kushiriki, na wawe tayari kufanya kazi ya ualimu wa usalama wa baisikeli baadaye. Kujua kiingereza ni nzuri ili kumwelewa Andrew vizuri. Tulikubali hela za UWABA za Wamba zitumikwe kulipa washiriki Tsh 5,000 kila siku pamoja kulipa chakula, kwa sababu washiriki watakuwa mbali na kazi na biashara zao.

Tulikubali kupata taarifa ya bei ya chakula kwenye canteen ya chuo cha usafirishaji na pia nje kwa mama lishe. Pia tuhakikisha booking ya darasa.

Ofisi

Mejah bado haja paka rangi ofisini mpya. Elaine aliandika baura kwa serekali za mtaa wa Manzese kutambulisha UWABA na ofisi yetu mpya na Juma atawapa.

Kodi

Juma alifuatalia na alipokea jibu la barua yetu kwa TRA kuomba taarifa ya kodi ya baisikeli. Inasema kwamba ushuru ya forodha ya baisikeli ni 25% kawaida lakini ni 0% kama inatoka Kenya au Uganda au kama inaingia kwenye format ya CKD (Completely Knocked Down). Hatuna uhakika CKD ina maana gani. Tulimpigia simu Bwana Ngaja wa kampuni wa guta na alisema analipa 25% ushuru wa forodha na 20% kodi ya ongezeko wa thamani (VAT), na anaingiza vifaa na siyo baisikeli nzima. Tuliamua kumpa nakala ya barua yetu kutoka TRA na pia kumpa nakala Mama Mlamba we halmashauri la jiji ambaye anapendelea swala hili.

Mambo ya hela

Wakati wa wiki Juma alitumia Tsh 1,500 kwa zawadi lakini Markus alikuwa ameshaondoka. Hela ya guta ya wiki hii bado haijalipwa. Juma ana Tsh 62,200 ya hela ya UWABA nyumbani. Wanachama walikubali kumpa Juma Chibaya Tsh 1,000 kununua dawa ya paa ya ofisi mpya.